

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI ARUSHA

Simu: +255 27 2508073/2503494
+255 27 2544330
+255 27 2545768



Mkurugenzi wa Jiji
20 Barabara ya Boma,
S. L. P. 3013,
23101 ARUSHA,

Barua Pepe: cd@arushacc.go.tz
Tovuti: www.arushacc.go.tz

Tarehe 24/04/2015

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UFAFANUZI WA TAMKO LA MKURUGENZI WA JIJI LA ARUSHA KUHUSU SAKATA LA VIDEO FUPI ILIYOTUMWA KATIKA MITANDAO YA KIJAMII BAINA YA MGANGA MFAWIDHI WA KITUO CHA AFYA NGARENARO NA VIONGOZI WA KAMATI YA SIASA YA CCM KATA YA LEVOLOSI JIJINI ARUSHA

Mnamo Tarehe 19/04/2019 ilirekodiwa video fupi ikionyesha majibizano baina ya mganga mfawidhi wa kituo cha afya Ngarenaro Dkt. Japhet Kivuyo na viongozi wa kamati ya siasa ya Ccm kata ya Levolosi Jijini Arusha kwa kile kilichodaiwa kuwa mganga huyo kutokuwepo katika eneo lake la kazi katika siku ya mapumziko ya sikukuu ya pasaka

Katika tamko lake alilolitoa Tarehe 22/04/2019 Mkurugenzi wa Jiji la Arusha Dkt. Maulid Suleiman Madeni alitamka kuwa amemsimamisha Dkt. Japhet Kivuyo kutekeleza majukumu yake kama Mganga Mfawidhi wa kituo na kuwa daktari wa kawaida kutokana na kauli aliyoitoa katika video ile kuwa sio lugha inayopaswa kutolewa na kiongozi hivyo nafasi yake kuchukuliwa na Dkt. David Mng'anya.

Kufuatia tamko hilo Mkurugenzi wa Jiji Dkt. Maulid Suleiman Madeni anakanusha uvumi unaonea katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuwa amemsimamisha kazi Dkt. Japhet Kivuyo bali amemtoa katika nafasi ya uongozi ili kupisha uchunguzi unaofanywa na Timu ya wataalamu iliyoundwa na Mkurugezi wa Jiji na uongozi wa Mkoa kuchunguza tukio hilo ili hatua stahiki ziweze kufuatwa.

IMETOLEWA NA;
OFISI YA MKURUGENZI
HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA